Usiruhusu Hisia Zako Zikapata Nafasi
(Don’t Let Your Feelings Get in the Way)

na

Ellis P. Forsman

Usiruhusu Hisia Zako Zikapata Nafasi

na

Ellis P. Forsman

Octoba 7, 2011

Usiruhusu Hisia Zako Zikapata Nafasi

2 Wafal 5:1-14

Mawazo ya mwanadamu katika kufanya kilicho chema:

- Amini moyo wako.
- Fuata moyo wako.
- Jiamini mwenyewe.

Kwa maneno, kuna imani isemayo hayupo mwenye msimamo. Hivyo, kilicho "sahihi" maana mtu anaweza "kuwa sio sahihi" kwa kila mmoja.

Kiuhalisia, Wakristo wanaofuata maandiko wanafahamu kuwa huu sio kweli.

Katika somo hili, tutaangalia yafuatayo:

- Jinsi ambavyo hisia zinavyoweza kupata nafasi ya kuishi kulingana ya kweli.
- Hisia zako zinaweza na zinaweza kuongozwa na msimamo mmoja wa ukweli wa Mungu.

Hisia zinawe kupata nafasi kwa njia ya kweli

Kila siku, wengi hujiita "Wakristo" wanaishi kwa ajili ya Bwana kulingana na "hisia zao." "Nina his…"; "Ninafikiri…"; "Ninaamini…"

Kauli kama kama hizi kimsingi zinamaana: haaziongozwi na neno la Mungu, lakini kwa sababu ya mawazo yao (kam "hisia").

Naaman (kiongozi aliyeheshimiwa katika Ashuru) – mtaifa aliyeongozwa na hisia zake:

2 Wafalme 5:1-14, "*Basi Naamani, jemaadari wa jeshi la mfalme wa Shamu, alikuwa mtu mkubwa mbele ya bwana wake, na mwenye kuheshimiwa kwa sababu kwa mkono wake BWANA alikuwa amewapa*

Washami kushinda; tena aalikuwa mtu hodari wa vita; lakini alikuwa mwenye ukoma. Na Washami walikuwa wametoka vikosi, wakachukua kijana mmoja mwanamke kutoka nchi ya Israeli; naye akamhudumia mkewe Naamani. Akamwambia bibi yake, laiti bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliyeko Samaria! Maana angemponya ukoma wake. Mtu mmoja akaingia akamwambia bwana wake, akasema yule kijana mwanamke aliyetoka nchi ya Israeli asema hivi na hivi. Mfalme wa Shamu akasema, haya basi, mimi nitampeleka mfalme wa Israeli waraka. Basi akaenda zake, akachukua mikononi mwake talanta kumi za fedha, vipande vya dhahabu elfu sita, na mavazi kumi. Akampelekea mfalme wa Israeli waraka ule, kusema waraka huu utakapokuwasilia, tazama nimemtuma mtumishi wangu Naamani kwako, ili upate kumponya uko wake. Ikawa mfalme wa Israeli alipousoma waraka, alirarua mavazi yake, akasema, je! Mimi ni Mungu, niue na kuhuisha, hata mtu huyu akanipelekea mtu nimponye uko wake? Fahamu basi nakusihini, mwone ya kuwa mtu huyu anataka kugombana nami. Ikawa, Elisha, yule wa Mungu, aliposikia kwamba mfalme wa Israeli ameyararua mavazi yake, ndipo akatuma mtu kwa mfalme akisema mbona umerarua mavazi yako? Na aje sasa kwangu mimi, naye atajua ya kuwa yuko nabii katika Israeli. Basi Naamani akaja na farasi wake na magari yake akasimama mlangoni pa nyumba ya Elisha. Naye Elisha akampeleka mjumbe akisema, enenda ukaoge katika yordani mara saba, na nyama ya mwili wako itakurudia naw utakuwa safi. Lakini Naamani akakasirika akaondoka akisema tazama nalidhania bila shaka atatoka kwangu, na kusimama na kuomba kwa jina lwa BWANA, Mungu wake na kupitisha mkono wake mahali penye ugonjwa, na kuniponya mimi mwenye ukoma. Je Abana na Farpari mito ya Dameski, si bora kuliko maji yote ya Israeli? Je siwezi kujiosha ndani yake na kuwa safi? Akageuka akaondoka kwa hasira. Watumishi wake wakamkaribia, wakamwambia wakasema baba yangu kama yule nabii angelikuambia kutenda jambo kubwa usingalilitenda? Je si zaidi basi akikuambia jioshe uwe safi? Ndipo akashuka akajichovya mara saba katika Yordani, sawasawa na neno lake yule mtu wa Mungu; nayo nyama ya mwili wake ikarudi ikawa kama nyama ya mwili wa mtoto mchanga, akawa safi."

Alijua kwamba angeponywa kutokana na ukoma wake.

2 Wafalme 5:2-3, "*Na Washami walikuwa wametoka vikosi, wakachukua mfungwa mmoja kijana mwanamke kutoka nchi ya Israeli; naye akamhudumia mkewe Naamani. Akawambia bibi yake laity bwana wangu angekuwa pamoja na yule nabii aliyeko Samaria! Maana angemponya ukoma wake.*"

Aliambiwa na Elisha (msemaji wa kweli wa Mungu) kujiosha katika Yordani mara saba. 2 Wafalme 5:10, "*Naye Elisha*

akampeleka mjumbe, akisema enenda ukaoge katika Yordani mara saba na nyama ya mwili wako itakurudia nawe utakuwa safi."

Badala ya kumuamini Elisha (nabii wa Mungu), aliondoka kwa kile alichodhani kingetokea.

2 Wafalme 5:11-12, "*Lakini Naamani akakasirika akaondoka akasema tazama nalidhania bila shaka atatoka kwangu na kusimama na kuomba kwa jina la BWANA, Mungu wake na kupitisha mkono wake mahali penye ugonjwa, na kuniponya mimi mwenye ukoma. Je Abana na Farpari mito ya Dameski, je si bora kuliko maji yote ya Israeli? Je siwezi kujiosha ndani yake na kuwa safi? Akageuka akaondoka kwa hasira.*"

Hataivyo, alipotimiza mapenzi ya Mungu alitakaswa (na akamtukuza Mungu).

2 Wafalme 5:15, "*Akamrudia yule mtu wa Mungu yeye na mafuatano wake yote. Akaja akasimama mbele yake akasema, sasa tazama najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli; basi nakuomba upokee mbaraka kwa mtumwa wako.*"

Gehazi (mtumishi wa Elisha) pia aliongozwa vibaya na kile alichodhani ni sawa.

2 Wafalme 5: 15-27, "*Akamrudia yule mtu wa Mungu yeye na mafuatano wake yote. Akaja akasimama mbele yake akasema, sasa tazama najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli; basi nakuomba upokee mbaraka kwa mtumwa wako. Lakini akasema kama BWANA aishivyo ambaye nimesimama mbele yake, sipokei kitu; akamshurutisha apokee lakini akakataa. Naamani akasema kama sivyo, lakini mtumwa wako na apewe mzigo wa udongo wa baghala wawili; kwa maana mtumwa wako hatatoa tena sadaka ya kuteketezwa wala dhabihu kwa miungu mingine, ila kwa BWANA. Jambo hili BWANA amwachilie mtumwa wako; bwana wangu akiingia nyumbani mwa Rimoni ili aabudu humo, naye akitegemea mkononi mwangu nami nikijiinama nyumbani wa Rimoni, hapo ninapojiinama nyumbani mwa Rimoni, BWANA amwachilie mtumwa wako jambo hili. Akamwambia enenda kwa amani basi akamwondokea mbali kidogo. Lakini Gehazi mtumishi wa Elisha mtu wa Mungu akasema tazama bwana wangu amemwachilia huyo Naamani Mshami asivipokee mikononi mwake vile vitu alivyovileta, kama BWANA aishivyo, mini nitamfuata mbio nipokee kitu kwake. Basi Gehazi akamfuata*

Naamani. Naye Naamani alipoona mtu apigaye mbio anakuja nyuma yake alishuka garini amlaki, akasemaa, Je! Ni amani? Akasema amani. Bwana wangu amenituma kusema tazama sasa hivi wamenijia kutoka milimani mwa Efraimu vijana wawili wa wana wa manabii; uwape nakuomba talanta ya fedha na mavazi mawili. Naamani akasema uwe radhi ukatwe talanta mbili. Akamshurutisha akafunga talanta mbili za fedha ndaani ya mifuko miwili, na mavazi mawili akawatwika watumishi wake wawili nao wakayachukua mbele yake. Naye alipofika kilimani alivitwaa mikononi mwao, akaviweka nyumbani; akawaacha wale watu kuondoka, nao wakaenda zao. Lakini yeye akaingia akasimama mbele ya bwana wake. Elisha akamwambia watoka wapi, Gehazi? Akanena, mtumwa wako hakuenda mahali. Akamwambia je moyo wangu haukuenda na wewe, hapo alipogeuka yule mtu katika gari ili akulaki? Je! Huu ndio wakati wa kupokea fedha, na kupokea mavazi, na mashamba ya mizeituni, na mizabibu, na kondoo, ng'ombe, na watumwa, na wajakazi? Basi ukoma wa Naamani utakushika wewe na wazao wako hata milele. Naye akatoka usoni pake mwenye ukoma kama theluji."

Alikuwa pamoja na Elisha wakati Naamani alipompa zawadi ya fedha.

2 Wafalme 5:15-16, "*Akamrudia yule mtu wa Mungu yeye na mafuatano wake yote. Akaja akasimama mbele yake akasema, sasa tazama najua ya kwamba hakuna Mungu duniani mwote, ila katika Israeli; basi nakuomba upokee mbaraka kwa mtumwa wako. Lakini akasema kama BWANA aishivyo ambaye nimesimama mbele yake, sipokei kitu; akamshurutisha apokee lakini akakataa.*"

Alafu, alifikiri/ alihisi kuwa na haki alipokwenda na kuomba fedha kwa Naamani.

2 Wafalme 5:20, "*Lakini Gehazi mtumishi wa Elisha mtu wa Mungu akasema tazama bwana wangu amemwachilia huyo Naamani Mshami asivipokee mikononi mwake vile vitu alivyovileta, kama BWANA aishivyo, mini nitamfuata mbio nipokee kitu kwake.*"

Matokeo: ukoma wa Naamani ulihamishiwa kwake.

- 2 Wafalme 5:25-27, "*Lakini yeye akaingia akasimama mbele ya bwana wake. Elisha akamwambia watoka wapi, Gehazi? Akanena, mtumwa wako hakuenda mahali. Akamwambia je moyo wangu haukuenda na wewe, hapo alipogeuka yule mtu katika gari ili akulaki? Je! Huu ndio wakati wa kupokea fedha,*

na kupokea mavazi, na mashamba ya mizeituni, na mizabibu, na kondoo, ng'ombe, na watumwa, na wajakazi? Basi ukoma wa Naamani utakushika wewe na wazao wako hata milele. Naye akatoka usoni pake mwenye ukoma kama theluji."

- 1 Tim. 6:10, "*Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengine hali wakiitamani hiyo wamefarakana na Imani, na kujichoma kwa maumivu mengi.*"
- Mit. 16:25, "*Kuna njia ionekanayo sawa kwa mwanadamu, lakini mwisho wake ni mauti.*"

Ubatizo na wokovu: Nahisi (Ninaamini, Ninafahamu, nk.) Nimeokolewa.

- Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na dunia, basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari.*"
- Marko 16:15-16, "*Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkaihuribiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa.*"
- Mdo. 2:38, "*Petro akwaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina la Yesu Kristo nanyi mtapata ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Mdo. 8:36-38, "*Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji; yule towashi akasema, tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana. Akajibu akasema, naamini ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi naye akambatiza.*"

Wengi wanaamini "hisia zao" na hivyo kuamini kwamba wameokolewa. Alafu, wengi hukataa kuamini kinachofundishwa na maandiko wanapo sikiliza au kuisoma.

Ushoga na ushafu: Ninahisi (Nianajua, nk) kwamba ushoga sio dhambi.

- Law. 18:22, "*Usilale na mwanamume mfano wa kulala na mwanamke; ni machukizo.*"
- Rum. 1:18-32, "*Kwa maana ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni juu ya uasi wote na uovu wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu. Kwa kuwa mambo ya Mungu yanayojulikana yamekuwa dhahiri ndani yao kwa maana Mungu aliwadhihirishia. Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana na kufahamika kwa kazi zake; yaani uweza wake wa milele na Uungu wake hata wasiwe na udhuru; kwa sababu walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo. Kwa ajili ya hayo Mungu aliwaacha katika tamaa ya mioyo yao, waufuate uchafu hata wakavunjiana heshima miili yao. Kwa maana waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa milele. Amina. Hivyo Mungu aliwaacha wafuate tamaa zao za aibu hata wanawake wakabadili matumizi ya asili kwa matumizi yasiyo ya asili.; wanaume nao vivyo hivyo waliyaacha matumizi ya mke, ya asili, wakawakiana tamaa, wanaume wakiyatenda yasiyopasa, wakapata nafsini mwao malipo ya upotevu wao yaliyo haki yao. Na kama walivyokataa kuwa na Mungu katika fahamu zao, Mungu aliwaacha wafuate akili zao zisizofaa, wayafanye yasiyowapasa. Wamejawa na udhalimu wa kila namna, uovu na tamaa na ubaya; wamejawa na husuda na uuaji, na fitina, na hadaa, watu wa nia mbaya wenye kusengenya. Senye kusingizia, wenye kumchukia Mungu, wenye jeuri, wenye kutabakari, wenye majivuni, wenye kutunga mabaya, wasio watii wazazi wao, wasio na ufahamu, wenye kuvunja maagano, wasiopenda jamaa zao, wasio na rehema; ambao wakijua sana hukumu ya haki ya Mungu, ya kwamba wayatendao hayo, wamestahili mauti, wanatenda hayo, wala si hivyo tu, bali wanakubaliana nao wayatendao.*"

- 1 Kor. 6:9, "*Au hamjui ya kuwa wadhalimu hawataurithi ufalme wa Mungu? Msidanganyike, waasherati hawatauridhi ufalme wa Mungu, wala waabudu sanamu, wala wazinzi, wala wafiraji, wala walawiti,*"

Wengi wanahisi ya kwamba walizaliwa wakiwa mashoga na kwamba Mungu asingemuumba mtu akiwa shoga kama isingekuwa dhambi.

Alafu, hawa (wanaopenda ushoga) hukataa ufunuo wa maandiko.

Bado, wengi wanakataa kwamba maandiko yanafundisha wanapo sikia na kuisoma.

Tuache ukweli uongoze hisia zetu

Ukweli ni wazi, haibashiri.

Ukweli unatoka kwa Mungu pekee.

- Yohana 1:1, "*Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye neno alikuwa Mungu.*"
- Yakobo 1:17, "*Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka.*"

Ukweli huja kupitia injili.

- Kol. 1:5, "*Kwa sababu ya tumaini mlilowekewa akiba mbinguni; ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya Injili;*"
- Efe. 1:13, "*Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu.*"

Wakristo, chini ya mamlaka ya Kristo ni lazima washikilie kweli yake.

- Gal. 1:6-10, "*Nastajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeiza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili*

yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mlioipokea, na alaniwe. Maana sasa je ni wanadamu ninaowashawishi au Mungu? Au nataka kuwapendeza wanadamu? Kama ningekuwa hata sasa nawapendeza wanadamu, singekuwa mtumwa wa Kristo."

- 2 Yohana 1:9-11, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu naye haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salamu. Maana yeye ampaye salamu azishiriki kazi zake mbovu.*"

Kwa upande mwingine hisia zetu, hubadilika.

Hivyo, tusipokuwa wagumu katika kweli, tunapaswa kumshukuru Mungu kwa ajili ya hisia zetu. hisia tulizonazo hutumika kama kipima upepo kama imetulia au kinyume na kweli yake.

Tukifanya vizuri, kutii kweli huleta furaha katika maisha yetu.

Mdo. 8:26-39, "*Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa. Naye akaondoka; mara akamwona mtu wa kushi, towashi mwenye mamlaka chini ya Kandake malkia wa Kushi, alieyewekwa juu ya hazina yake yote; naye alikuwa amekwenda Yerusalemu kuabudu, akawa akirejea akawa ameketi garini akisoma chuo cha nambii Isaya. Roho akamwambia Filipo sogea karibu na gali hili, ukashikamane nalo. Basi Filipo akaenda mbio, akamsikia anasoma chuo cha nabii Isaya, akanena je yamekuelea hayo unayosoma? Akasema nitawezaje kuelewa mtu asiponiongoza? Akamsihi Filipo apande na kuketi pamoja naye. Na fungu la maandiko alilokuwa akilisoma ni hili, aliongozwa kwenda machinjoni kama kondoo, na kama vile mwana kondoo alivyo kimya mbele yake amkataye manyoya, vivyo hivyo yeye naye hafunui kinywa chake. Katika kujidhili kwake hukumu yake iliondolewa. Ni nani atakayeeleza kizazi chake? Kwa maana usima wake umeondolewa katika nchi. Yule towashi akamjibu Filipo, akasema, nakuomba nabii huyu asema maneno haya kwa habari ya nani; ni habari zake mwenyewe au za mtu mwingine? Filipo akafunua kinywa chake naye akianza*

kwa andiko lilo hilo, akamhubiri habari njema za Yesu. Wakawa wakiendelea njiani, wakafika mahali penye maji, yule towashi akasema tazama maji haya ni nini kinachonizuia nisibatizwe? Filipo akasema ukiamini kwa moyo wako wote inawezekana . akajibu akanena, naamini ya kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Akaamuru lile gari lisimame, wakatelemka wote wawili majini, Filipo na yule towashi naye akambatiza. Kisha walipopanda kutoka majini, Roho wa Bwana akamnyakua Filipo, yule towashi asimwone tena; basi alikwenda zake akifurahi."

Tusipofanya vizuri, dhambi inalala mlangoni.

Mwa. 4:4-13, "*Habili naye akaleta akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama BWANA akamstakabali Habili na sadaka yake; bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhabika sana, uso wake ukakunjama sana, BWANA akamwambia Kaini, kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? Kama ukitenda vyema, hutapata kibali?"Usipotenda vyema dhambi yako inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. Kaini akamwambia Habili nduguye, twende uwandani. Ikawa walipokuwapo uwandani, Kaini akamwinukia Habili nduguye, akamwua. BWANA akamwambia Kaini, yuko wapi habili ndugu yako? Akasema sijui mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?akasema umefanya nini sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. Basi sasa umelaniwa wewe katika ardhi iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. Kaini akamwambia BWANA adhabu yangu imenikulia kubwa haichukuliki.*"

Lakini hata tukitenda dhambi, tunaweza kutubu na kufurahi tena.

Luka 15:11-24, "*Akasema mtu mmoja alikuwa na wana wawili, yule mdogo akamwambia babaye, baba nipe sehemu ya mali inayoniangukia. Akawagawia vitu vyake. Hata baada ya siku si nyingi, yule mdogo akakusanya vyote akasafiri kwenda nchi ya mbali; akatapanya mali zake huko kwa maisha ya uasherati. Alipokuwa amekwisha kutumia vyote, njaa kuu iliingia nchi ile, yeye naye akaanza kuhitaji. Akaenda akashikamana na mwenyeji mmoja wan chi ile, naye alimpeleka shambani kwake kulisha nguruwe. Akawa akitamani kujilisha kwa maganda waliyokula nguruwe, wla hapana mtu aliyempa kitu. Alipozingatia moyoni mwake, alisema, ni watumishi wangapi wa baba*

yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, baba nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena; nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Akaondoka akaenda kwa babaye. Alipokuwa angali mbali, baba yake alimwona akamwonea huruma, akaenda mbio akamwangukia shingoni akambusu sana. Yule mwana akamwambia baba nimekosa juu ya mbingu na mbele yako; sistahili kuitwa mwana wako tena. Lakini baba aliwaaambia watumwa wake. Lileteni upesi vazi lililo bora, mkamvike, mtieni na pete kidoleni, na viatu miguuni. Mleteni ndama yule aliyenona mkamchinje; nasi tule na kufurahi; kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka, alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia."

Hitimisho

Naamani alijifunza kutokana na makosa yake ya kuamini katika hisia zake wakati Gehazi akilipa kwa ajili yake.

Tunatakiwa kujifunza kutoka kwa hawa watu kwa ukweli wa Mungu unapaswa kutuongoza kwa njia ambayo tunapaswa kwenda, na "hisia" zetu iwe ni matokeo ya kuamini katika ukweli wake.